Fikranet Connect—Vol 3



Dickson John

*You Can Rise Again*

# UNAWEZA INUKA TENA

## Tumaini Jipya, Nguvu ya kutokata Tamaa.

## KUHUSU MWANDISHI

Dickson John ni mwandishi wa vitabu mbalimbali vya ujasiriamali na mwalimu elimu binafsi za maisha. Uandishi ni ndoto ambayo amekuwa nayo tangu zamani na hivi sasa ameamua kuiweka katika vitendo.

Miongoni mwa vitabu alivyoviandika ni pamoja na:-

- Kiwanda Mkononi.
- Fanikisha Ndoto Yako.
- Una nini Mkononi?
- Unaweza inuka Tena.

## Yaliyomo

1. kuhusu mwandishi .......................................................... 1
2. wakfu ............................... **Error! Bookmark not defined.**
3. shukrani ........................... **Error! Bookmark not defined.**
4. Kuna Kuinuka Tena Baada Ya Kuanguka............................ 3
5. Maeneo Yenye Athari Na Maumivu Katika Maisha........ **Error! Bookmark not defined.**
6. Ni Nini Kilichokufanya Kuanguka?.......**Error! Bookmark not defined.**
7. Saikolojia ya binadamu katika changamoto na athari zake**Error! Bookmark not defined.**
8. Maadui Wanaoweza Kukufanya Usiinuke.**Error! Bookmark not defined.**
9. Unaweza Inuka Tena.......... **Error! Bookmark not defined.**

Rejea ............................... **Error! Bookmark not defined.**

## KUNA KUINUKA TENA BAADA YA KUANGUKA.

.........................................

Katika kila jambo kuna majira yake, na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu. Wakati wa kuzaliwa, na wakati wa kufa; *wakati wa kupanda*, na wakati wa *kung'oa yaliyopandwa*; wakati wa kuua, na wakati wa kupooza; wakati wa kubomoa, na wakati wa kujenga; *wakati wa kulia*, na *wakati wa kucheka*; wakati wa kuomboleza, na wakati wa kucheza; *wakati wa kutupa* mawe, na *wakati wa kukusanya* mawe; wakati wa kukumbatia, na wakati wa kutokumbatia; *wakati wa kutafuta*, na *wakati wa kupoteza*; wakati wa kuweka, na wakati wa kutupa; wakati wa kurarua, na wakati wa kushona; wakati wa kunyamaza, na wakati wa kunena; wakati wa kupenda, na wakati wa kuchukia; wakati wa vita, na waakati wa amani. Kila kitu kimefanywa kizuri kwa wakati wake.

Kila mara tunakutana changamoto ambazo zinatutoa katika malengo ya maisha. Katika maisha kuna watu watatu ambao wakikuondokea, maisha huanza upya. Watu hawa huwa ni muhimu sana katika maisha ya mtu. Watu hao ni Baba au Mama, Mke au Mume. Mmoja kati ya watu hawa anapoondoka basi mfumo wa maisha ya mtu huathirika kwa namna moja ama nyingine, kusimama inategemeana na misingi binafsi ambayo mtu huyu atakuwa amejiwekea yeye mwenyewe.

Pamoja na mambo haya yote, kitabu hiki kina ujumbe muhimu sana kwa ajili yako. Ni ujumbe wa amani kwako. Yamkini watu wengine wamekwambia "*Huwezi kuinuka tena*" kutokana na changamoto unazozipitia. Watu wengine wamekudhihaki na kukucheka sana, na wemeonyesha dharau hadharani mbele zako. Haya yote ni

changamoto unayopitia. Kuna namna unaweza kuinuka tena, kuinuka tena na kuinuka tena.

Nilipokuwa nikisoma BIBLIA huku nikitafakari nilikutana na ujumbe mmoja ambao ulinisukumu kuandika kitabu hiki kwa ajili ya kuwatia moyo vijana wenzengu wa rika mbalimbali. Nilisoma vitabu viwili tofauti ambavyp ndivyo vitakuwa msingi wa kitabu hiki. Kuna mtu mmoja katika kitabu cha Biblia aitwaye Ayubu, Kwa wakristo wanajua hadithi yake, namna ambavyo alipitia changamoto ambazo kwa kipindi hiki tulichonacho hakuna mtu ambaye angelisimama kama yeye, ingawaje mateso yake yalikuwa yakihusiana na Imani, lakini kuna jambo la kujifunza kutoka kwake. Kwa kifupi Ayubu alikuwa ni mtu mchaji wa Mungu, alimwamini Mungu kwa kiwango kikubwa. Ilifikia siku moja shetani alitoka ili kumjaribu Ayubu, akamjaribu kwa kila namna alivyoweza, akaua mifugo yake yote, akaua watoto wake wote. Na kila kitu alichokuwa nacho. Alipitia mateso mengi lakini jambo tunajifunza kutoka kwake, hakukata tamaa, aliinuka tena.

Katika kitabu hicho cha Ayubu 22:29 tunakuta maneno muhimu sana ambayo ndiyo msingi wa kitabu hiki na ndipo jina la kitabu linapokea, imeandikwa hivi *"Hapo watakapokuangusha, utasema kuna KUINUKA TENA……."* kuna kuinuka tena baada ya kuanguka, kuna kuinuka kibiashara, kuna kuinuka tena baada ya anguko la muda mrefu. Amini na tumia maneno haya kutoka katika kitabu cha MIKA 7:8 "*…… Niangukapo, nitainuka tena"* Mungu ana wazo zuri tu juu yako, na msingi wa ushindi wa mwanadamu umejengwa katika kuinuka kila mara anapoanguka.

Tutanguka mara hata ishirini ili kujenga ndoa yenye mahusiano imara. Tutaanguka mara mia ili kutimiliza lengo moja tu la kuuza kitabu au biashara kwa ufanisi. Kuanguka ni sehemu ya maisha ya mwanadamu, lakini ni namna gani unakabiliana na hali hii kila inapotokea? Je unaamani kuna kuinuka tena baada ya kuanguka? Ndio mimi naamini juu ya kuinuka tena katika kufanya jambo Fulani, siwezi acha kuandika vitabu vya kuelimisha jamii na kuwapa maarifa kwa kisa eti watanzania hawasomi vitabu, licha ya kwamba sifikii malengo ya uuzaji wa kitabu lakini nitaendelea kufanya hivyo kila siku kadri ninavyojaliwa na mwenyezi Mungu.

Kila anguko lina mafunzo ndani yaake, inamaanisha kuna sehemu fulani ambapo unakosea kila mara ndio maana unaanguka. Inakupa nafasi ya kujichunguza, kujipima na kukupa uwezo wa kuamua upya ili kuinuka kila unapoanguka. Amini unaweza kuimuka tena itakupa nguvu ya kuinuka tena. Kuna watu ambao wamekata tamaa kwamba hawawezi kutoka katika umaskini, najua umekuwa na jitihada nyingi za kutaka kutoka mahali ulipo, kila mara unapojaribu unaanguka, hebu kiri maneno haya "*Niangukapo, Nitainuka tena*" hata kama wengine watashindwa kusimama, wewe simama.

Ikiwa njia moja imeshindikana, kuna njia nyingine itafunguka kwa ajili yako. Usione kukosa elimu kubwa kama ni kigezo pekee cha kukufanya kushindwa kuendelea na maisha. Watu wengine wamekuwa na taratibu za kujinyonga pindi matokeo yao yanapokuwa mabaya katika mitihani yao ya mwisho, wameona kana kwamba njia yao imefungika, hakuna namna ya kuweza kutoka. Unadhani elimu kwako ina manufaa kuliko maisha na uhai wako? Wangapi wamesoma na bado wapo mtaani wanafanya shughuli ambazo hata haziendani na elimu yao. Hata kama ukifeli shule kuna kuinuka tena yawezekana ikawa njia ile ile ama njia nyingine. Usijinyonge kwa kudhani kwamba utakuwa umetatua matatizo, hujui huko uendako utakutana na nini, hivyo basi endelea kutumia zawadi ya uhai kutoka kwa Mungu.